**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**


*Simu*: +255-26-2323189
*Barua pepe*: ps@moha.go.tz
*Tovuti*: www.moha.go.tz

Mji wa Serikali - Mtumba,
Mtaa wa Habari/Afya,
S. L. P 2916,
40483 DODOMA.


**13 Novemba,2023**

## TAARIFA KWA UMMA

## UTEKELEZAJI WA TANGAZO LA MSAMAHA KWA USALIMISHAJI WA SILAHA HARAMU KUANZIA TAREHE 1/9/2023 HADI 31/10/2023

Mtakumbuka kuwa tarehe 28/8/2023 nilitoa Notisi ya Msamaha wa kutoshitakiwa kwa yeyote atakayesalimisha silaha haramu kwa hiari kuanzia tarehe 01/09/2023 hadi tarehe 31/10/2023. Notisi hii ilitangazwa kupitia **Tangazo la Serikali Na. 619** la tarehe 25/08/2023 ambalo liliainisha masharti ya usalimishaji wa silaha kwa hiari.

Hatua hiyo ya kutangaza msamaha wa usalimishaji wa silaha haramu ilitokana na sababu zifuatazo:-

a) Utekelezaji wa Makubaliano ya Wakuu wa Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika ya kutenga mwezi Septemba kila Mwaka kuwa ni mwezi wa Msamaha wa usalimishaji wa silaha haramu kwa hiari hadi mwaka 2030. Makubaliano hayo yalifanyika katika kikao cha 29 cha Kawaida jijini Adis Ababa Ethiopia tarehe 3-4 Julai, 2017.

b) Mamlaka niliyonayo kisheria chini ya kifungu cha 64 cha Sheria ya Udhibiti wa Silaha na Risasi ya Mwaka 2015 Sura ya 223 kuhusu kutoa Notisi ya Msamaha wa kutoshitakiwa kwa wale wote watakaosalimisha silaha haramu kwa hiari kwa kuzingatia masharti yaliyoko kwenye Notisi hiyo.

Katika Notisi hiyo masharti ya msamaha wa usalimishaji wa silaha haramu kwa hiari yalikuwa kama ifuatavyo:-

i. Kipindi cha Msamaha wa Usalimishaji wa silaha kilikuwa kuanzia tarehe 1/09/2023 hadi 31/10/2023
ii. Silaha zilitakiwa zisalimishwe katika maeneo yafuatayo:-
   a. Kwenye Kituo chochote cha Jeshi la Polisi.
   b. Ofisi za Serikali za Mitaa,
   c. Ofisi za Watendaji wa Kata/Shehia
iii. Muda wa kusalimisha silaha ulikuwa kuanzia saa mbili asubuhi (2:00) hadi saa kumi jioni (10:00)

Jeshi la Polisi kupitia Vyombo vya habari vikiwemo redio, televisheni, semina na mikutano ya hadhara, liliendesha kampeni ya kuwahamasisha wananchi ili wajitokeze kusalimisha silaha haramu kwa hiari. Kampeni hizo ziliendeshwa kwa kushirikiana na Kamati za Usalama, Viongozi wa Serikali za Mitaa, Watendaji Kata, Madiwani na Viongozi wa Dini.

Matokeo ya usalimishaji wa silaha haramu hadi kufikia tarehe 31/10/2023 ni kwamba Jumla ya silaha haramu zilizosalimishwa ni **301** kwa mchanganuo wa PISTOL **04**, S/gun **51** , Rifle **07** ,$G_3$ **01** na Gobore **238** pia risasi **262** za aina mbalimbali zilisalimishwa.

Mchanganuo wa usalimishaji wa silaha haramu kimikoa ni kama ifuatavyo:-

a) Tanga -silaha **138**
b) Dodoma-silaha **76**
c) Singida-silaha **19**
d) Morogoro-silaha**18**
e) Mkoa wa Kipolisi Rufiji- **12**
f) Pwani –silaha **10**
g) Songwe- silaha **9**
h) Rukwa- silaha **6**
i) Manyara –silaha **3**
j) Kinondoni –Silaha **3**
k) Njombe –silaha **2**
l) Geita – silaha **1**
m) Arusha – silaha **1**
n) Ilala –silaha **1**
o) Mbeya-silaha **1**
p) Tabora-silaha **1**

Kufuatia matokeo haya ya usalimishaji wa silaha haramu nalielekeza Jeshi la Polisi kufanya yafuatayo:-

a. Kufanya misako kwa kutumia taarifa za kiintelelijensia ili kuwabaini na kuwakamata wale wote wanaomiliki silaha kinyume na Sheria na kisha kuwachukulia hatua za kisheria.

b. Kufanya misako kwa kutumia taarifa zilizopo ili kuwabaini wale wote wanaojihusisha na utengenezaji wa magobore na kuwachukulia hatua za kisheria kwani kwa mujibu wa takwimu za silaha zilizosalimishwa imeonekana magobore kuwa na idadi kubwa.

c. Kufanya mapitio ya Sheria na Kanuni zilizopo kuhusu Udhibiti wa Silaha ili kuona kama ipo haja ya kuzifanyia marekebisho kwa lengo la kuimarisha udhibiti

Nitumie nafasi hii kuwashukuru wananchi wote waliojitokeza na kusalimisha silaha haramu kwa hiari katika kipindi cha Msamaha yaani mwezi Septemba na Oktoba 2023. Pia nawashukuru Viongozi wa Dini pamoja na Kamati za Usalama kuanzia ngazi ya Mtaa, Kata, Wilaya na Mkoa kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi katika kipindi cha Kampeni za Usalimishaji wa silaha haramu kwa Hiari.

Kwa namna ya pekee, natoa shukrani kwa Vyombo vya habari vyote nchini vikiongozwa na Shirika la Utangazaji Tanzania ( TBC) iliyoandaa Kipindi Maalum, kwa kushiriki kikamilifu katika kuwafikishia wananchi ujumbe kuhusu msamaha wa usalimishaji wa silaha jambo ambalo limefanya Jeshi la Polisi kuendesha Kampeni kwa urahisi.

Aidha, napenda kuwahakikishia Umma wa Watanzania kuwa silaha ambazo zimesalimishwa katika kipindi cha msamaha zitateketezwa hadharani kwa tarehe itakayo tangazwa, lengo likiwa ni kuepusha madhara ambayo yanaweza kujitokeza kwa raia na rasilimali za Taifa kutokana na uwepo wa silaha haramu.

Nitoe wito kwa wananchi, kuendelea kutoa taarifa kwa Jeshi la Polisi kuhusu watu wanaomiliki silaha kinyume na Sheria ambapo Jeshi la Polisi litaratibu taarifa hizo na kuchukua hatua stahiki ikiwa ni pamoja na kutunza siri za watoa taarifa.

Pia niwaombe wananchi kuendelea kusalimisha silaha zilizokuwa zinamilikiwa kihalali kutokana na sababu ya mmiliki kufariki, changamoto ya kiafya au uzee. Hii itasaidia silaha zilizokuwa zinamilikiwa kihalali kutoangukia mikononi mwa wahalifu.

Aidha, nitumie nafasi hii kuwakumbusha wananchi wanaomiliki silaha kihalali kuzingatia taratibu za kisheria kuhusu umiliki wa silaha kwa kuhifadhi silaha sehemu salama na kuepuka kuonyesha silaha hadharani ili kutoleta madhara na taharuki kwa wananchi.

Mhandisi Hamad M.Y Masauni (Mb)

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI**

**13 NOVEMBA, 2023**